

IN THE HIGH COURT OF ZANZIBAR

HOLDEN AT VUGA

CIVIL CASE NO. 40 OF 2012 (OS.)

BAHATI UBWA

PLAINTIFF

VERSUS.

1. KATIBU MTENDAJI

KAMISHENI YA WAKF NA MALI YA AMANA

ZANZIBAR

2. MRAJIS WA NYARAKA – ZANZIBAR -----

DEFENDANTS.

H U K U M U.

Rabia H. Mohamed, J.

Hii ni Kesi ya Madai (O.S.) iliyofunguliwa Chini ya Order X Rules 6 na 8 za Sheria ya Mwenendo wa Madai Sura ya 8.

Mdai ni BAHATI UBWA na Wadaiwa ni KATIBU MTENDAJI KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA, ZANZIBAR na MRAJIS WA NYARAKA ZANZIBAR, ambae hajawahi kufika Mahkamani licha ya kupokea wito kwa ajili hiyo.

Katika Madai yake hapa Mahkamani, Mdai ameiomba Mahkama izingatie mambo yafuatayo:-

- a. Mahkama imuamuru kufutwa kwa Hati ya Wakf katika Nyumba ya Mdai Nam. 22/70 iliyopo Miembeni waliyoandikiwa, JAMILA UBWA JAHA, SHOOKO UBWA JAHA, MSIM UBWA JAHA, SAUMU UBWA JAHA, MITHLETI UBWA JAHA (Ambao wote kwa sasa ni Marehemu), na ADAM MOH'D (yuhai). Hati hiyo ya Wakf Nam. 9/98 ya tarehe 21/12/1998 iliyotayarishwa na Mdaiwa Nam. 1 iliyosajiliwa na Mdaiwa Nam. 2 tarehe 11/11/1998 kwa Nam. 149/1998 katika Vol. I, Book A-3.
- b. Mahkama imuamuru Mdaiwa Nam. 1 kutayarishwa hati nyengine ya Wakf kwa Nyumba ya Mdai Nam. 22/70 iliyopo Miembeni kwa majina ya ADAM MOH'D FAIZI, na THANIA MOH'D FAIZI, na Mdaiwa Nam. 2 apewe amri ya kuisajili hati hiyo mpya ya Wakf mara itakapotayarishwa na Mdaiwa Nam. 1.
- c. Amri nyengine yo yote itakayokuwa ya manufaa kwa Mdai.

Katika maelezo yake hapa Mahkamani Mdai ameieleza Mahkama kwamba aliamua kuweka Wakfu Nyumba yake Nam. 22/70 baada ya kuwa na hali mbaya ya kiafya kwa muda wa miaka minane. Kutokana na kutokuwa tayari nyumba hiyo kuuzwa baada ya yeye kufariki. Kwa sababu hii basi alitayarisha Wakfu lakini badala yake yeye mwenyewe pamoja na mnufaika mmoja tu wa Wakf, yaani ADAM MOH'D FAIZI ndio wapo hai. Wanufaika wengine watano wa Wakfu huo tayari wameshafariki. Waliofariki aliwataja ni JAMILA UBWA JAHA, SHOOKO UBWA JAHA, MSIM UBWA JAHA, SAUMU UBWA JAHA na MITHLETI UBWA JAHA.

Kwa vile mnufaika aliyebakia katika Wakfu anaishi nje ya nchi Mdai anaiomba Mahkama hii imkubalie kufuta Wakfu aliouweka katika Nyumba Namba 22/70 ya Miembeni na badala yake utengenezwe Wakfu mpya utakaojumuisha majina ya THANIA MOH'D FAIZI na ADAM MOH'D FAIZI, hasa kwa vile THANIA ni mkaazi wa Zanzibar ambae atakuwa ni Muangalizi wa nyumba hiyo.

Kwa mujibu wa Mdai na Kielelezo P2, Warka wenye usajili Namba 2/98 uliosajiliwa tarehe 21/2/98 baada ya kumalizika kizazi chote cha wanufaika wa Wakfu, hiyo nyumba Namba 22/70 iliyopo Miembeni Wakfu uende katika Msikiti wa Miembeni.

Mdaiwa Namba 1 hakuwa na pingamizi kwa hati hii ya Wakfu kufutwa na kutolewa nyengine mpya itakaojumuisha wanufaika wake ADAM MOH'D FAIZI na THANIA MOH'D FAIZI, kama tu hakutakuwa na pingamizi kutoka Msikiti wa Miembeni. Imamu wa Msikiti wa Miembeni alipoitwa Mahkamani hapo hakuwa na pingamizi na ombi la kufutwa Wakfu na kutolewa mpya kwa vile bado nyumba yenyewe ipo kwenye dhima ya wenye Wakfu.

Kwa mujibu wa Hati ya Wakfu iliyotolewa na Mdai (P2) ni hati ya Wakf ambayo haitengui lakini kwa vile anachokusudia kukifanya Mdai ni kuongeza tu mnufaika wa Wakfu huu. Hivyo basi hasa kwa kuzingatia kwamba pande zote mbili za dai hili hazipingani na dai hili. Mahkama hii haina budi kukubaliana na dai la Mdai. Dai la Mdai linakubaliwa. Kila upande wa kesi hii utabeba gharama zake.

Sgd: Rabia H. Mohamed

Judge

27/3/2013.

MAHKAMA:

Hukumu imesomwa leo tarehe 27/3/2013 mbele ya Mdai tu.

Sgd: Rabia H. Mohamed

Judge

27/3/2013.

Ninathibitisha kuwa hii ni Nakala halisi ya Hati ya Asili.

Sgd. **GEORGE J. KAZI**

MRAJIS

MAHKAMA KUU

ZANZIBAR.

